

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO



Unapojibutafadhali taja:

Kumb.Na.KTV/NDC/P.30/2/55

23.08.2024

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo amepokea Kibali cha Ajira Mpya kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia Barua yenye Kumb.Na.FA.97/228/01/09 ya tarehe 25.06.2024. Hivyo, anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa zakujaza nafasi zifuatazo:

1.0. MPISHI DARAJA LA II (NAFASI 01)

1.1.1 KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kufanya usafi wa jiko;
- ii. Kupika vyakula vya aina mbalimbali;
- iii. Kuhakikisha vyombo vya kupikia vinakuwa safi
- iv. Kutayarisha orodha ya vyakula vya mlo kamili(balanced diet);
- v. Kupika vyakula vya kitaalamu;
- vi. Kuhakikisha chakula kinaandaliwa kwa muda muafaka;
- vii. Kuahakikisha usalama wa jiko na chakula na
- viii. Kutekeleza majukumu mengine utakayopangiwa na msimamizi wako

1.1.2 SIFAZAMWOMBAJI.

Awe amehitimu kidato cha nne (IV). Awe na Astashahada/Cheti (Technician Certificate) ya fani ya Mapishi (Food Production/ Culinary Arts) kutoka Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

1.1.3 NGAZIYAMSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya Serikali TGS C

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI


- i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45 isipokuwa wale walioko kazini Serikalini;
- ii. Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuhainisha kwenye Mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishiwa Umma;
- iii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wakuaminika.
- iv. Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma na wamejipatia Sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitisha barua zao za maombi ya nafasi ya kazi kwa waajiri wao na waajiri wajiridhishe ipasavyo;
- v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa **kuzingatia sifa za kazi husika. Certificates, -Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV na VI, -ComputerCertificate;**
- vi. "Testmonial ", "Provisional Results ", "Statement of results ", hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita (**FORM IV RESULTS SLIPS**) **HAVITAKUBALIWA.**
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika (**TCU, NECTA na NACTE**).
- viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi;

- ix. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na.CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba,2010.
- x. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xi. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 29.08.2024.
- xii. **MUHIMU:**Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyo sainiwa pamoja na vyeti vya elimu,anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

**Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo,
S.L.P 688,
Mpanda-Katavi**

- xiii. Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (RecruitmentPortal) kupitia anuani ifuatayo; <https://portal.ajira.go.tz/> (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa('RecruitmentPortal').
- xiv. Maombi yatakayo wasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Tangazo hili limetolewa na:


Eng. Stephano B. Kaliwa,
MKURUGENZI MTENDAJI (W),
NSIMBO.